Usharia wa Itikafu

Kufanya itikafu ni katika matendo yaliyo bora sana, na twa'a tukufu. Kutoka kwa A'isha Mungu awe naye radhi anasema: "Alikuwa Mtume ﷺ akifanya itikafu (maisha yake) katika kumi la mwisho wa mwezi wa Ramadhani mpaka Mungu alipomkabidhi roho yake (Mtume alipokufa)" [Imepokewa na Bukhari.].

Na inaruhusiwa ki-sheria kwetu sisi na kwa waliokuja kabla yetu kufanya itikafu, Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na tulimusia Ibrahimu na Ismaili Itakaseni nyumba yangu kwa ajili ya wale wanaoizunguka kwa ajili ya kutufu na wanaokaa hapo na (kwa ajili ya) wanaorukuu na kusujudu hapo pia") (Al-Baqarah –Aya 125).

https://www.al-feqh.com/sw/itikafu

al-feqh.com/sw